**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA DR. SWARE I.SEMESI (MB), KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge,*
*Toleo la Januari, 2016*

---

## I. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, nitoe shukrani kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniamini na kunipa madaraka ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii. Sambamba na hilo ni washukuru viongozi wote wa chama kwa ushirikiano wanaonipatia

katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge na pia majukumu ya kichama.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu kwa kunitia moyo na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kupambana na mazingira magumu ya kisiasa katika mkoa ninakotakiwa kufanyia kazi zangu za kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kiujumla. Sekta hizi zimeendelea kutoa mchango mkubwa ikiwemo kuwa **chanzo cha kipato kwa zaidi ya 65% ya Watanzania, kuhakikisha usalama wa chakula, kuchangia pato la taifa kwa zaidi ya 28% na mauzo ya nje kwa zaidi ya 24%**.

**Mheshimiwa Spika,**Japo sekta hizi ni muhimu ila zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri ukuaji wake. Changamoto hizo zinajumuisha: *utengaji na utoaji mdogo wa fedha za bajeti ya maendeleo; upungufu mkubwa wa maafisa ugani, watalaam na watafiti; miundombinu duni* (*ikiwemo ya utoaji wa taarifa za tahadhari);* na *upungufu wa viwanda vya kuchakata bidhaa zake.*

**Mheshimiwa Spika***,* Athari za mabadiliko ya tabianchi zinaongeza changamoto hizo ikiwemo: *kuongezeka kwa ukame na magonjwa ya mimea na mifugo; mvua*

*zisizotabirika; kuingia kwa maji ya chumvi katika mashamba na vyanzo vya maji baridi; mafuriko* na *uharibifu wa mashamba na miundombinu ya kilimo, ufugaji na uvuvi ikiwemo mazalia ya samaki.*

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa kwa **mwaka 2015** ukuaji wa shughuli za kilimo (*mazao, ufugaji, misitu na uwindaji*) umepungua na kufika **2.3% kutoka 3.4% kwa mwaka 2014. Pia kiwango hicho ni kidogo kwa wastani wa ukuaji wa 3.2% kwa kipindi cha mwaka 2010 - 2013**. **Mwenendo huu ni mdogo sana ukilinganisha na shabaha ya 6%** iliyoweka nchini chini ya **MKUKUTA II** na kuelekezwa na **CAADP** na **TAFSIP**.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imependa tathmini iliyofanywa na taasisi za wadau wa kilimo kwa mwenendo wa bajeti ya wizara ya(za) kilimo, mifugo na uvuvi kwa kipindi cha **miaka kumi (10) iliyopita (2007/2008 – 2016/2017) na kuona kuwa** si wakuridhisha japokuwa sekta hizi kutoa mchango mkubwa sana kwa taifa. Takwimu zinaonesha kuwa **wastani wa bajeti za wizara za sekta hizo kwa kipindi hicho ni 2.2% tu ya bajeti ya taifa**. Kiwango hiki ni kidogo sana ukilinganisha na lengo la kufika 10% kama Serikali ilivyoridhia katika '*Azimio la Malabo*'. Kwa kipindi cha **miaka mitano ya kwanza (2007/2008 – 2011/2012)** wastani ulikuwa ni **2.7% tu,** wakati kwa kipindi cha **miaka mitano ya mwisho (2012/2013 – 2016/2017)** wastani ulikuwa ni **1.8% tu**.

- **Kilimo na Ushirika (*Fungu 43*)** imepata wastani wa TZS 250bilioni ambayo ni sawa na 1.8% tu ya bajeti ya taifa kwa kipindi cha mwaka **2007/2008 – 2016/2017**. Kati ya wastani huo, bajeti ya maendeleo ilipata wastani wa **TZS 80.3bilioni** ambayo ni **sawa na 32% tu ya bajeti ya kilimo na ushirika** na **1.6% ya bajeti ya maendeleo taifa**.

- **Mifugo na Uvuvi (*Fungu 99 na 64*)** imepata wastani wa **TZS 57.1bilioni ambayo ni sawa na 0.4% tu ya bajeti ya taifa** kwa kipindi cha mwaka **2007/2008 – 2016/2017**. Kati ya wastani huo, bajeti ya maendeleo ilipata wastani wa **TZS 20.7bilioni** ambayo ni sawa na **36% tu ya bajeti ya mifugo na uvuvi** na **0.4% ya bajeti ya maendeleo taifa**[1].

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, kama kweli kauli mbiu ya Tanzania ya viwanda kuwa na uhalisia inabidi kuongeza bajeti kwa sekta nzima ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi), kinyume na hapo kauli mbiu hiyo itaendelea kuwa kwenye vyombo vya habari tu.

[1] Policy Forum, Forum CC, Oxfam na TGNP- Taarifa ya uchambuzi kwa sekta ya kilimo kwa miaka 10

## II. KILIMO: Fungu 43

### a. Hali ya Kilimo Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama nchi bado tuna mapungufu makubwa kwa jinsi tunavyopanga mipango yetu. Sisi kama wabunge ambao kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali tunaweza kushindwa kutekeleza jukumu hilo la msingi kutokana na ukweli kwamba mipango inayoletwa na Serikali haitupi ni namna gani tuipe ushauri,kwani haina kipimo (target) kwa kila mwaka wa bajeti badala yake ina malengo ya miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika,** kama wabunge tunaendaje kukagua utekelezaji wa miradi bila kuelewa kwa kipindi hicho, utekelezaji wake ulitakiwa kuwa umefikia wapi kwa kulinganisha na fedha zilizotolewa na Bunge?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imeanza kwa utangulizi huo kwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/17, sehemu ya Kilimo kifungu cha 3.2.3.3 kinaonesha kuwa; *"Lengo ni kuhakikisha uwepo wa chakula cha kutosha na upatikanaji wa uhakika wa malighafi za uzalishaji katika viwanda vya mazao ya kilimo,mifugo na uvuvi.*

**Mheshimiwa Spika,** Lengo hilo ni zuri lakini halina kipimo yaani "indicators" ambacho waheshimiwa wabunge wanaweza kukitumia wakati wa kukagua miradi ambayo

inakuwa imetengewa fedha kwenye bajeti. Hoja ya msingi ni mpango lazima uoneshe wazi kazi itakayofanyika kulingana na fedha iliyopangwa, kinyume cha hapo ni kutoa mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za walipakodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kama inataka matumizi yanayofanyika yaendane na thamani ya fedha ni muda mwafaka sasa mipango iwe wazi ili waheshimiwa wabunge watoe ushauri unaoendana na hali halisi ya mipango husika. Mfano mzuri ni hizi skimu za umwagiliaji ambazo miaka yote inawekwa kwenye bajeti lakini ni nani anayefahamu kwa uhakika kuwa kiasi kilichotengwa ndicho kilichotengeneza kwa kiwango kinachoonekana kwa skimu husika kwa mwaka huo wa bajeti? Yaani ***"value for money"***

**Mheshimiwa Spika**, Mapungufu hayo pia yanajitokeza kwenye mpango wa miaka mitano, kwani mpango huo hauoneshi kwa kipindi cha kila mwaka Serikali itakuwa imetekeleza nini ili ipimwe kwa mpango wake huo badala yake inataka kupimwa kwa kipindi chote hadi mwaka 2020, wakati bajeti inapitishwa kila mwaka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba haya ni mapungufu makubwa ya Serikali na hivyo basi kutoa mwanya wa kupimwa na kukosolewa katika utendaji kazi wake.

**Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2015 umepungua kufikia asilimia 2.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 katika mwaka 2014 kwa shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao, ufugaji na uvuvi. Shughuli hizo zimekua na kupungua kwa asilimia 2.2, 2.4, 2.5 na 2.6 mwaka 2015 kwa mfuatano wa sekta tajwa ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.0, 2.2, 2.0, na 5.1 ya mwaka 2014.

**b. Migogoro ya Rasilimali Ardhi kati ya Wakulima, Wafugaji na Hifadhi**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania inakabiliwa na migogoro mikubwa kati ya watumiaji wa ardhi, migogoro hii inatokana na ukweli kwamba idadi ya watumiaji inaongezeka kwa kasi kubwa wakati eneo la ardhi ni lile lile. Katika kutambua suala hili, waheshimiwa wabunge katika Bunge la kumi (10) baada ya kutokea migogoro na mauaji baina ya watumiaji wa ardhi na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla (Mb),mnamo tarehe 01 Novemba, 2013 akatoa Hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge. Kwa hoja hiyo na Bunge lililazimika kuunda Kamati Teule iliyoongozwa na Mhe. Christopher Olenyokie Ole-Sendeka, (Mb) kama Mwenyekiti na wajumbe wengine wanne kati ya watatu

ni  ni wabunge katika Bunge hili la kumi na moja (11), na iliwasilisha taarifa yake Bungeni tarehe 2 Februari,2015.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha wa hotuba hii ya Kambi Rasmi nitayafanyia marejeo baadhi ya mapendekezo ya taarifa hiyo ambayo ilitoa ufafanuzi wa kina lakini utekelezaji wa maazimio yaliyowekwa bado Serikali imekaa kimya.

**Mheshimiwa Spika**, kamati hiyo ilionesha dhahiri migogoro inapoanzia kuwa ni;

a. Vijiji kutokuwa na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi,
b. Kutokutengwa kwa Maeneo Mahsusi kwa ajili ya Kilimo na Ufugaji.
c. Kutotengwa kwa maeneo mahsusi kwa ajili ya malisho
d. Kilimo na Ufugaji wa kuhamahama
e. Kutambua umuhimu na thamani ya ardhi na kuongezeka kwa mahitaji ya Ardhi kunakosababishwa na:
    i. Ongezeko kubwa la idadi ya watu na idadi ya mifugo,
    ii. Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya shughuli za ufugaji,
    iii. Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya kilimo,
    iv. Upanuzi wa maeneo ya hifadhi za Taifa,
    v. kupanuka na kuanzishwa kwa miji mipya,

vi. Ongezeko la vitalu vya uchimbaji madini na uwindaji,
vii. Kupungua kwa ardhi inayofaa kwa uzalishaji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, haya yote yapo kwenye sera na sheria mbalimbali za Serikali, lakini kila kimoja kinaona kina haki zaidi ya mwenzie na hapo ndipo tatizo linapozidi kuwa kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mdogo ni pale kati ya maeneo tajwa linapogundulika lina madini na mwekezaji akapatikana ni dhahiri wakaazi katika eneo husika haki zao zinaishia hapo na inawalazimu kuhama, na kama eneo hilo lilikuwa ni nyanda za malisho maana yake wafugaji wanahamia eneo lingine bila kujali matumizi yake ni ya aina gani. Pia tatizo lingine ni pale Watu wachache kumilikishwa maeneo makubwa ya ardhi na pengine kuanza kuyakodisha kwa wakulima wadogo na wafugaji kwa bei kubwa na hivyo kuzusha migogoro baina ya makundi hayo matatu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati ilibaini kuwa zaidi ya asilimia 25 ya eneo la Nchi ni hifadhi, hivyo Bunge liliazimia Serikali kutekeleza mambo yafuatayo, kwa muktadha wa wizara hii;

i. Kuyaachia mapori ya Serikali ambayo yamekosa sifa, ili yatumike kwa kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi.

ii. Migogoro wanayokumbana nayo wafugaji kutokana na kuingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi pamoja na kero nyingine inatokana na kukosekana kwa miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mrejesho maazimio tajwa hapo juu yametekelezwa kwa kiwango gani? kwani hadi sasa migogoro baina ya wafugaji, wakulima na hifadhi imekuwa ikiendelea na wananchi wamepoteza mali zao na wengine kupoteza uhai wao.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kurejea tena Sera na sheria zinazohusu matumizi ya raslimali ardhi, kwani wakati zinatungwa idadi ya watumiaji wa raslimali hiyo haikuwa kama ilivyo kwa sasa. Tuangalie idadi ya watanzania kwa sasa na miaka 50 au 100 ijayo watakuwa wangapi, Idadi ya mifugo na watumiaji wengine wa rasilimali hii ya ardhi.

### c. Hali ya Chakula Nchini

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula uliendelea na ununuzi wa nafaka katika kanda ya Songea, Makambako na Sumbawanga ambako kulikua na uzalishaji wa ziada. Wakati wa kuanza mwaka tarehe 1 Julai 2015 NFRA ilikuwa na tani 353,702.25 za nafaka. Hadi kufikia tarehe 14 Aprili 2016 NFRA ilikuwa imenunua tani 22,335.157 na kufanya akiba katika maghala yake kufikia tani 65,275.155 ambapo mahindi ni tani 61,315.586, mpunga ni tani 3,939.630 na mtama ni tani 19,890. Akiba hii imeiwezesha Serikali kukabiliana na uhaba wa chakula na maafa hususan mafuriko yaliyojitokeza nchini katika sehemu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya utekelezaji ya wizara inaonesha takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2015/2016 na upatikanaji wa chakula 2016/17 kuwa ni tani 16,172,841 zikilinganishwa na tani 15,528,820 za msimu wa 2014/15 kati ya tani hizo nafaka zilikuwa ni tani 9,457,108 na mazao yasiyo ya nafaka tani 6,715,733. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa mahitaji ya chakula kwa msimu wa 2016/17 ni tani 13,159,326 kati ya hizo mahitaji ya nafaka yalikuwa ni tani 8,355,767 na tani 4,803,560 isiyo nafaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa taarifa hiyo inaonesha kuwepo kwa ziada ya chakula ya tani 3,013,515 na hivyo taifa kuwa na utoshelevu kwa silimia 123 ikilinganishwa na

asilimia 120 kwa mwaka 2015/16. Palepale tunaambiwa pamoja na uzalishaji wa zaida Halmashauri 55 zilikuwa na ukosefu wa chakula, na jumla ya watu 1,186,028 walikuwa na mahitaji ya jumla ya tani 35,491.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa maelezo yanatakiwa kutolewa na Serikali kuhusu takwimu hizo za ziada ya tani 3,013,515 inawezekanaje Halmashauri 55 zikawa na upungufu wa chakula? Na kama kuna ziada ya nafaka tani 1,101,341 inakuwaje bei ya mahindi inazidi kupanda kila siku?

**Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kwamba January 2017, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alitoa kauli iliyoonesha kwamba wilaya 55 kati ya 169 zikiwemo za Zanzibar zilikuwa zinakabiliwa na upungufu wa chakula na hivyo zilikuwa zinahitajika tani 35,491 za chakula kati ya mwezi February hadi April 2017 na watu wapatao 1,186,028 walikuwa wanakabiliwa na njaa katika wilaya tajwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa toka kipindi tajwa hapo juu hadi sasa ni dhahiri kuwa wakulima bado hawajavuna mazao yao hivyo ni ukweli ulio wazi kuwa watanzania wengi zaidi wanakabiliwa na tatizo la njaa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ripoti ya utafiti iliyotolewa na taasisi ya Twaweza ya March, 2017 inaonesha kuwa; "Hali ya upungufu wa chakula

imeonekana kuwa mbaya zaidi katika miezi ya hivi karibuni. Hii inajidhihirisha pale ambapo kaya zilizoripoti kupata hofu ya kukosa chakula zilipanda kutoka asilimia 45 hadi asilimia 65 kati ya Septemba 2016 na Februari 2017. Vivyo hivyo, idadi ya kaya zilizopungukiwa na chakula ziliongezeka kutoka asilimia 43 Septemba 2016 hadi asilimia 51 Februari 2017. Kaya ambazo zilikuwa na angalau mtu mmoja aliyeshinda siku nzima bila kula nazo ziliongezeka kutoka asilimia 21 hadi asilimia 35 katika kipindi hicho hicho. Upungufu huu wa chakula umesababishwa kwa kiasi fulani na umasikini wa kipato unaofanya kaya maskini ziwe katika hali tete".

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania "monthly economic review" ya mwezi January 2017 zinaonesha kwamba bei ya mahindi imepanda kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Habari zilizoelezwa na wananchi ni kwamba upungufu wa chakula ni tatizo kubwa kwa sasa na hii ilijidhihirisha pale ambapo wahojiwa wengi wa Sauti za Wananchi (asilimia 78) waliripoti upungufu wa chakula katika maeneno waliyokuwa wakiishi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa utafiti wa bei za mazao ya vyakula uliofanywa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini na kuripotiwa na vyombo vya habari unaonesha kuwa;

Wilaya ya Kilombero, "Mfuko wa kilo 25 za sembe ulikuwa unanunuliwa Sh 18,000, sasa umepanda mpaka Sh 35,000," na bei hiyo ya kilo hizo 25 za sembe uuzwa mjini, lakini kwa wilayani imefika hadi Sh 40,000.

Soko kuu la Arusha; kilo moja ya unga wa sembe na dona inauzwa kati ya Sh 1,600 na 1,800, wakati debe moja la mahindi likiuzwa Sh 15,000 na gunia la kilo 100 Sh 90,000 hadi 110,000. Mchele unauzwa Sh 2,200 hadi 2,400 kwa kilo moja, huku mazao mengine kama ngano, maharagwe, mbaazi na kunde nayo yakipanda bei.

Wilayani Longido, wananchi wanalazimika kubadilishana mbuzi mmoja mkubwa mwenye thamani kati ya sh 40,000 na 50,000 kwa debe moja la mahindi.

Mkoa wa Dodoma, bei ya mchele ilikuwa kati ya Sh 1,200 na 1,400 kwa kilo moja mkoani Shinyanga, ikiwa ni bei ya jumla huku wao wakiuza kwa Sh 1,500 hadi 1,600 bei ya rejareja.

Mkoa wa Mtwara, mfuko wa kilo 25 wa unga wa sembe unauzwa Sh 40,000 badala ya Sh 27, 000 bei ya msimu wa awali.

Mkoa wa Ruvuma, mkoa ambao unazalisha mahindi kwa kiwango kikubwa hapa nchini na ni moja ya "the big four"kwenye uzalishaji wa mahindi. Kilo moja ya mahindi inauzwa wastani wa Sh 730 na 750.

Mkoa wa Njombe, debe moja la mahindi linauzwa kati ya shilingi 18,000/- na 22,000/- na mkoa huo ni wazalishaji wakubwa wa mahindi.

Mkoa wa Tanga, bei ya gunia moja la mahindi Tanga mjini linauzwa kati ya shilingi 95,000/- hadi shilingi 97,000/- badala ya shilingi 67,000/- za awali na Mfuko wa sembe wa kilo 25 ulikuwa ukiuzwa kati ya shilingi 25,000/- na 24,000/- lakini hivi sasa unauzwa shilingi 30,000/- hadi 27,000/- na ile ya kilo 50 iliyokuwa ikiuzwa shilingi 50,000/- na shilingi 55,000/- hivi sasa inauzwa hadi shilingi 60,000/-. Mkoa wa Mwanza, bei ya gunia la mahindi linauzwa kati ya shilingi 100,000/- na 125,000/-.

Wilaya ya Ukerewe, Gunia la mahindi linauzwa kati ya shilingi 105,000/-na 120,000/- tofauti na mwaka jana ambapo lilikuwa linauzwa kati ya shilingi 70,000/- na 80,000/-.

Wilaya ya Bunda mkoani Mara, imepanda kutoka shilingi 14,500/- kwa debe moja hadi

kufikia shilingi 20,000/-, huku unga wa muhogo ukipanda kutoka shilingi 12,500/- hadi 17,500/-. Nafaka nyingine kama mtama zimepanda kutoka shilingi 10,000/- hadi 17,500/- kwa debe, wakati ulezi unauzwa shilingi 30,000/- kwa debe moja.

**Mheshimiwa Spika,** kupanda kwa bei ya chakula, je, jukumu la serikali ni nini? na jukumu ya NFRA ni nini?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Kilimo na vitengo vyake kuhakikisha kwamba watanzania kwa ujumla wao muda wote wanakuwa na uhakika wa kupata chakula, mengine yanafuatia. Hivyo basi kitendo cha watanzania kukosa chakula ni dalili kwamba kuna mapungufu ya kiutendaji sehemu fulani.

### d. Mabadiliko ya Tabianchi na Sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi yana madhara ya moja kwa moja kwa kilimo, mifugo na uvuvi na sekta hii wahusika wakubwa ni wananchi wa hali ya chini na ya kati.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabia nchi yanaonekana dhahiri nchini Tanzania, uzalishaji wa kilimo unatishiwa na hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi kutokana na matukio kama mafuriko na ukame. Mabadiliko ya tabia nchi ni tishio kubwa zaidi la kimazingira kwa maisha hapa duniani, linaloathiri

mazingira yetu, sio tu kiuchumi, lakini pia kijamii na kitamaduni. Tanzania imekuwa ikikabiliwa na vipindi vya ukame vinavyotokea mara kwa mara ambavyo vimeathiri shughuli za kilimo na kusababisha uhaba wa chakula.

**Mheshimiwa Spika**, Utafiti juu ya athari za mabadiliko ya tabia ya nchi katika maeneo ya wilaya za Iramba mkoani Singida na Meatu mkoani Simiyu na namna ya kukabiliana nao kwa mtazamo wa kijinsia katika kilimo na maliasili yamebaini; mvua zisizotabirika, magonjwa ya wanyama na mazao pamoja na magonjwa ya binadamu. Hii hali imepelekea zaidi ya asilimia 80 ya watu kuwa masikini huku kaya zinazoongozwa na wanawake zikiwa maskini zaidi kuliko zinazoongozwa na wanaume. Utafiti huo uliofanyika kwa kipindi cha miaka mitano tangu mwaka 2011 hadi 2015, ukiongozwa na Dk. Samwel Kabote Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

**Mheshimiwa Spika,** Katika jumla ya **kazi 142** zinazotarajiwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18, ni kazi **12 tu** ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha **TZS 25.5bilioni ambayo ni sawa na 17% tu**.

**Mheshimiwa Spika, Kati ya kazi 12** zilizoainishwa kuwa na uhusiano na mabadiliko ya tabianchi, ni kazi moja (1) tu

ndio ina kiwango cha ‘Juu’ cha uhusiano wakati kazi kumi na moja (11) zina kiwango cha ‘Chini’ na hakuna hata moja yenye kiwango cha ‘Kati’. *Maudhui yake katika mabadiliko ya tabinchi – Kupunguza (Mitigation), Kukabiliana (Adaptation),na Vyote viwili.* Pia, uchambuzi unaonesha kuwa **kati ya kazi 12** zilizoainishwa kuwa na uhusiano na mabadiliko ya tabianchi, kazi tisa (9) zina maudhui ya ‘Kukabiliana (Adaptation)**’** na kazi tatu (3) zina maudhui ya ‘Vyote viwili (Both)**’** na hakuna kazi yoyote yenye maudhui ya ‘Kupunguza (Mitigation)[2]’

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mifugo fungu 99 tika jumla ya **kazi 27** zinazotegemewa kutekelezwa, ni **kazi tisa (9) tu ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi**. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha **TZS 1.4bilioni ambayo ni sawa na 36%**.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya jumla ya **kazi 23 za Wizara kwa fungu 64** zinazotegemewa kutekelezwa, ni **kazi tano (5) tu ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi**. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha **TZS 1.5bilioni ambayo ni sawa na 19% tu ya fungu hilo**.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hii ni hatari kwa maendeleo ya nchi yetu na sekta nzima ya uzalishaji, kwani kila uzalishaji unategemea mabadiliko ya tabianchi.

[2] Forum CC –taarifa ya tathmini ya Bajeti ya Kilimo 2017/18

**Mheshimiwa Spika,** Serikali na vyombo vyake inawajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba, wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo ambao ndio wazalishaji wakuu wanapatiwa taaluma ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi mashambani.

**Mheshimiwa Spika**, tafiti zinaonesha kwamba wakulima wadogo bado wanalima bila ya kufuata sera za sekta mbalimbali kinachozingatia mabadiliko ya tabia nchi, maana yake ni kwamba dhana nzima ya kilimo na ufugaji unaozingatia mabadiliko ya tabia nchi bado ni dhana mpya katika mipango yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani, inasema kwamba sasa ni muda mwafaka japokuwa tumechelewa kama nchi kuhamasisha wakulima wadogo kujihusisha na Kilimo Kinachozingatia Mabadiliko ya Tabianchi na kuwe na Programu za kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika jamii. Ili kufikia lengo hilo ni lazima kuongeza motisha na vichocheo miongoni mwa wadau wa mabadiliko ya tabia nchi kushirikishana na kuchangia uzoefu wao katika mchakato wa kutayarisha programu za maendeleo ya kilimo-***District Agricultural Development Programmes*** (DADPs).

### e. Upatikanaji wa Mbegu na Mbolea

**Mheshimiwa Spika**,tangu mwaka 2009 Serikali imekuwa na miradi kadhaa iliyozinduliwa ili kufanya Mapinduzi katika kilimo kwa kuhimiza uwekezaji binafsi katika kilimo program kadhaa zilinduliwa ambazo ni; programu ya SAGCOT mwaka 2010; Jukwaa la Kilimo Afrika (Grow Africa Forum) mwaka 2011; Mpango wa Uwekezaji wa Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania (TAFSIP), Mpango wa Taifa wa Uwekezaji Tanzania chini ya CAADP mwaka 2011; Matokeo Mkubwa Sasa' (BRN) mwaka 2013, kuanza kwa utekelezaji wa Mfuko wa Kuchochea Kilimo wa SAGCOT mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika,** mapinduzi hayo yote kiini chake ni kuhakikisha wakulima wanatumia mbegu bora na mbole sahihi katika uzalishaji. Programu hizo tajwa zimekuja na Makampuni ya Kimataifa ya mbegu kuingia kwa nguvu kubwa kwenye soko la pembejeo, yakilenga mbegu zenye faida (hasa mahindi chotara na baadhi ya aina za mpunga), biashara ambayo ilitegemea kwa sehemu kubwa mbegu zinazoagizwa kutoka nje. Makampuni ya Pioneer Hi-Bred, Monsanto na Syngenta kwa sasa ndio makampuni makubwa zaidi ya nje. Kampuni nyingine za mbegu za ukanda wa Afrika pia zinafanya biashara nchini Tanzania, ambazo ni pamoja na East Africa Seed Company (Kenya), FICA (Uganda) na MRI (Zambia, ambayo kwa sasa inamilikiwa na Sygenta). Kampuni ya Mbegu ya Kenya (KSC) pia ipo nchini Tanzania kupitia

kampuni zake tanzu za Simlaw (mboga) na Kibo Seed[3]. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hii ni kuweka reahani kilimo chetu.

**Mheshimiwa Spika,** Makampuni Makubwa ya Kimataifa huelekeza rasilimali zao na muda kwenye mazao machache yanayoweza kuwapatia faida kubwa. Masoko madogo kwa ajili ya mbegu za kienyeji au zile ambazo zimebadilishwa kwa kawaida hayahudumiwi[4], Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ni muhimu sana kuhakikisha mbegu zetu za asili zinalindwa na ili zisije zikapotea kabisa na hivyo kupoteza urithi wetu wa mbegu za asili.

### f. Upatikanaji wa mbegu

**Mheshimiwa Spika**, Mbegu kwa ajili ya kilimo hupatikana kutokana na mifumo wa ugavi rasmi na isiyo rasmi (pia hujulikana kama mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima); asilimia 90 hutokana na mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima wakati asilimia 10 hutokana na sekta rasmi ya mbegu.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya mbegu ya mwaka 2003 haitambui kwa uwazi *mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima(sekta ya mbegu isiyo rasmi)* na aina za

---

[3] Kubadili Sheria Za Mbegu Na Ulinzi Wa Aina Za Mbegu Na Mimea Nchini Tanzania— The African Centre for Biosafety, April 2016-

[4] The African Centre for Biosafety,March 2015

mbegu za kienyeji na haisemi chochote kuhusu haki za wakulima.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta rasmi ya mbegu nchini Tanzania husambaza kiasi kidogo sana cha mbegu bora kwa wakulima nchini Tanzania (takribani asilimia 4-10) lakini bado ndiyo inayopata uungwaji mkono mkubwa wa serikali, fedha na taratibu za udhibiti huku mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima ambao hutoa asilimia 90, inabaki kutotambuliwa na haipati msaada.

**Mheshimiwa Spika,** Utafiti uliofanywa na ACB mwaka 2014 huko Morogoro na Mvomero uligundua kwamba zaidi ya asilimia 80 ya mbegu za asili za mahindi, mazao aina ya kunde na mpunga zinazotumika na wakulima hazijathibitishwa, na wakulima wengi huendelea kutumia kwa kurudia mbegu zinazotokana na mavuno ya msimu uliopita.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taarifa ya utekelezaji ya Wizara inaonesha kuwa makadirio ya mahitaji ya mbegu kwa mwaka ni tani 60,000 za mbegu bora. Aidha, Randama inaonesha kuwa wakala wa mbegu za kilimo (ASA) umeongeza uzalishaji wa mbegu bora za nafaka na mikunde toka tani 2,804 msimu wa 2015/2016 hadi tani 2,884 msimu wa 2016/17. Uzalishaji wa ndani

wa mbegu ni sawa na asilimia 4.81 tu ya nahitaji ya mbegu kwa nchi kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** maana yake ni kwamba asilimia 95.19 ya mahitaji ya mbegu kwa mwaka zinaingizwa na makampuni yanayojihusisha na mbegu toka nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ijitafakari kuhusiana na hali hii ya mbegu kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa; usambazaji wa mbegu uzingatie na uende sambamba na aina ya mbegu (breed) ambazo zinazingatia aina ya hali ya hewa (microclimate) na hali ya udongo katika maeneo husika.

### g. Upatikanaji wa Mbolea

**Mheshimiwa Spika,** takwimu za Serikali zinaonesha kuwa mahitaji ya mbolea kwa mwaka ni tani 485,000,aidha takwimu zinaonesha kuwa hadi mwezi machi,2017 tani 297,000 ziliingizwa nchini na tani 140,000 zilitolewa(ziliuzwa) nje ya nchi.
Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hapa kuna tatizo kubwa katika utendaji wetu, kama mahitaji yetu ni makubwa na hayatimizwi lakini bado tunatoa mbolea ndani na kupeleka nje ya nchi. Tatizo ni aina ya mbolea inayopelekwa nje haina ubora unaotakiwa kwa wakulima wetu? Kama ndio ni kwanini uzalishaji unakuwa

upo chini ya viwango kukidhi matakwa ya wakulima/ kilimo chetu?

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto kubwa linaloikabili sekta ndogo ya mbolea ni mfumo wa usambazaji ambao hauna uhakika kuendana na mahitaji ya wakulima kulingana na misimu ya kilimo na hivyo mbolea inapofikishwa kwa wakulima muda stahiki wa matumizi unakuwa tayari umeishapita.

**Mheshimiwa Spika,** ruzuku ya mbolea imekuwa ni kichaka kikubwa cha wizi wa fedha za Serikali kwa muda mrefu, lakini kilimo hakioneshi kuwa kinakua. Kwa msimu wa kilimo 2015/16 Serikali ilitoa vocha za ruzuku 2,999,778 kwa wakulima 999,993 zenye thamani ya shilingi bilioni 78.1 au dolla za Marekani milioni 36.4[5].

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa ruzuku kwa njia moja au nyingine unavunja nguvu mfumo wa kibiashara wa mbolea, na kwa kuwa mfumo wa usambazaji wa mbolea ni shida, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuuimarisha mfumo wa kibiashara ili muda wote wa mwaka mbolea iwepo madukani. Ni dhahiri wakulima sio kama hawana uwezo wa kununua mbolea, bali wanachohitaji ni upatikanaji wa uhakika wa mbolea katika maeneo yao.

[5] East African Business Week, November 24,2015

**h. Tathmini ya Utekelezaji wa Programu ya kuendeleza sekta ya Kilimo awamu ya kwanza (ASDP-I)**

**Mheshimiwa Spika,** program ya ASDP ni program ya miaka 15 inayotekelezwa kwa awamu, na awamu ya kwanza ilikuwa ni ya miaka 7 ilianza mwaka wa fedha (2006/07 – 2012/13) na ilimalizika mwezi wa Juni 2013. ASDP1 ili lenga kukuza kilimo kufikia asilimia 6 kwa mwaka na hivyo kilimo cha wakulima wadogo kuwa na tija zaidi katika mazingira ya ushindani kibiashara. Programu nzima ilitarajiwa kutumia jumla ya USD Milioni 315.6 sawa na UA Milioni 210. Kati ya fedha hizo, hadi program inamalizika Serikali na wachangiaji wengine walitoa jumla ya UA Milioni 146.564 na kubakiza UA 64236,000 tu.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa hiyo program unasaidia miradi ya kitaifa kwa matumizi ya program za sekta ya kilimo zilizo chini ya Wizara ya kilimo, shughuli zilizo ngazi ya wilaya na vijiji zinazosaidiwa chini ya mfumo wa Local Government Deveolopment Grant uliokuwa unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa Programu hii ya awamu ya kwanza mafanikio yapo, lakini pia mapungufu yapo, moja wapo ya mapungufu ni kuchelewa kutolewa kwa fedha katika utekelezaji wa miradi na hivyo kusababisha gharama za utekelezaji wa miradi kupanda. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza

kwamba dhana nzima ya umiliki katika miradi ya DADPS inayotekelezwa katika ngazi za wilaya kushuka chini, uelimishaji wananchi unatakiwa kuwa mkubwa sana katika awamu ya pili ya ASDP ili kutimiza malengo ya miradi inayoibuliwa na wananchi.

### i. Mpango wa SAGCOT

**Mheshimiwa Spika**,mpango wa SAGCOT unahusisha vijiji 359 vilivyo katika wilaya 30 zilizo katika mikoa 8 vinakadiriwa kuwa na eneo lenye ukubwa wa hekta 6,131,771 sawa na asilimia 60 ya ardhi yote iliyo katika mpango wa SAGCOT ni ardhi ya vijiji, na asilimia 2 ni ardhi ya jumla na asilimia iliyobakia ni maji na eneo la hifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Kamati teule ya Bunge iliyowasilisha taarifa yake humu Bungeni mwezi wa februari, 2015 inaonesha kuwa migogoro mikubwa ya vijiji kuporwa ardhi na taasisi za Serikali, pamoja na wawekezaji ni mingi kwenye vijiji vya wilaya za Kilombero, Bagamoyo, Rufiji, Chunya, mbalali, Sumbawanga.

Wilaya hizo zote ni sehemu ya wilaya 30 za mpango wa SAGCOT, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kama mitafaruku ya ardhi ipo katika vijiji husika kwa mujibu wa taarifa ya kamati teule ya Bunge iliyoongozwa na Mhe Christopher Ole Sendeka, je mpango huo si unatashindwa kuwa na manufaa kwa wananchi katika maeneo yenye migogoro? Na kama maeneo yatatwaliwa bila ridhaa ya vijiji husika, je ule mkakati wa **"nucleus-outgrowers model"** utafanyaje kazi? Kwani wananchi/ wanavijiji wengi si watakuwa ni manamba katika mashamba hayo ya SAGCOT?

**Mheshimiwa Spika,** ni muda mwafaka sasa kwa Bunge kupata mrejesho wa maazimio yake yaliyotokana na ***"Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini".***

## III. MAPITIO YA BAJETI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kupitia fungu 43 kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilitengewa jumla ya Shilingi **206,816,421,000/-**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **174,103,348,000/-** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi **32,713,073,000/-** ni fedha za maendeleo. Hadi mwaka huo wa fedha unamalizika Wizara ilipokea shilingi **2,663,428,542/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani na

shilingi **5,035,062,321/-** zikiwa ni fedha za nje, na hivyo kufanya jumla ya fedha za maendeleo kwa fungu 43 zilizopokelewa kwa mwaka 2015/16 kuwa shilingi **7,698,490,863/-** sawa na asilimia 23.53 ya fedha za maendeleo zilizopitishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2016/17 Fungu 43 lilitengewa jumla ya Shilingi **210,359,133,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **109,831,636,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **100,527,497,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Fedha za maendeleo zilizoongezwa ni fedha za madeni ya wakandarasi wa skimu za miradi ya umwagiliaji na hivyo kuifanya jumla ya fedha za maendeleo kuwa shilingi **101,527,497,000/-**. Fedha za ndani zilikuwa shilingi **23,000,000,000/-** na fedha za nje shilingi **78,527,497,000/-** Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fedha zilizokuwa zimetolewa na shilingi **2,251,881,250/**- sawa na **asilimia 2.22** tu na kati ya fedha hizo fedha za ndani zilikuwa shilingi **1,382,191,924/-** na fedha za nje shilingi **349,081,000/-**

**Mheshimiwa Spika,** kama fedha za maendeleo/miradi hazipo, iwaje kuna fedha za OC? matumizi yake ni nini?

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2017/18 wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **216,019,071,000/-** kati ya fedha hizo shilingi **151,456,312,000/-** ni fedha za

maendeleo, ambazo ni ongezeko la shilingi **49,928,815,000/-** Kwa kulinganisha na maombi ya mwaka wa fedha 2016/17. Kambi Rasmi ya Upinzani baada ya kupitia kitabu cha Maendeleo –Juzuu ya IV fedha za maendeleo kwa fungu 43 inaonesha jumla ya shilingi **150,253,000,000/-** na hivyo kufanya tofauti kati ya Taarifa ya Wizara na ile ya Hazina kuwa shilingi **1,203,312,000/-**. Hii ni tofauti kubwa sana na kwa vyovyote vile tunaomba maelezo ya nini kimetokea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 inaonesha kuwa bajeti kwa ajili ya maendeleo ya kilimo (fungu 43) zitengwe shilingi bilioni **1,134.07/-** na Mifugo (fungu 99) ilitarajiwa kutengewa jumla ya shilingi bilioni **156.52/-**, na Uvuvi (fungu 64) shilingi bilioni **1,024.78/-,** hivyo kuifanya sekta nzima ya kilimo kama inavyosomeka kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kuwa shilingi bilioni **2,314.99/-**. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwanini mpango wa miaka mitano uliopitishwa na Bunge hili hili haufuatwi katika utekelezaji?

**Mheshimiwa Spika**, Makusanyo kwa mwaka 2016/17, sekta ya Kilimo ilikuwa shilingi **2,903,760,494.43/-**. Makusanyo haya ni ya chini kabisa ukilinganisha na sekta ya Uvuvi (Fungu 64) shilingi **10,321,908,868.10/-**, na sekta ya Mifugo (Fungu 99) ilikusanya shilingi **21,756,818,934.30/-**. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni

inaitaka Serikali kuweka na kusimamia malengo na vipaumbele vyake kiuhalisia kwani Kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu.

## IV. SEKTA YA MIFUGO: Fungu 99

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya mifugo ni muhimu sana kwani ina mchango asilimia 4.4 kwa pato la taifa,pia inahudumia takriban 10% ya watanzania wanaoishi kwa kutegemea mfumo huu wa ufugaji na Kutoa ajira kubwa hasa mijini- machinjio mbalimbali, mabucha, vifaa vitokanavyo na ngozi, kutunza maliasili wanyama, utalii na mazingira nk.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2015/2016, idadi ya mifugo nchini ilifika ng'ombe milioni 25.8, mbuzi milioni 17.1 na kondoo Milioni 9.2. Pia, wapo kuku wa asili milioni 42.0, kuku wa kisasa milioni 34.5 na nguruwe milioni 2.67.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi hicho uzalishaji wa maziwa ulikuwa ni lita bilioni 2.14. Aidha, usindikaji wa maziwa ulikuwa ni lita 167,620. Pia, uzalishaji wa mitamba katika kipindi hicho ulifikia mitamba 11,449. Kati ya mitamba hiyo, 646 ilizalishwa kutoka mashamba ya Serikali na Kampuni ya Ranchi za Taifa-NARCO na 10,803 kutoka sekta binafsi. Aidha, dozi 80,000 za mbegu bora za uhimilishaji zilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji ambapo ng'ombe 221,390 walihimilishwa.

**Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia 8.54 kutoka tani 597,757 (ng'ombe 319,112; mbuzi na kondoo 124,745; nguruwe 54,360; na kuku 99,540) mwaka 2014/2015 hadi tani 648,810 (ng'ombe 323,775; mbuzi na kondoo tani 129,292; nguruwe tani 91,451; na kuku tani 104,292) mwaka wa 2015/2016. Pia, uzalishaji wamayai kwa mwaka 2015/2016 ni mayai bilioni 4.35 ikilinganishwa na mwaka 2014/15. Aidha, mifugo iliyouzwa minadani ni ng'ombe 1,470,805, mbuzi 1,161,840 na kondoo 253,243 wenye thamani ya shilingi bilioni 976.474 kwa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na thamani ya shilingi bilioni 1,027.4 ya waliouzwa mnadani mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 5.22

**Mheshimiwa Spika**, VAT kwenye mazao ya mifugo inabidi kuondolewa kwani kodi hii inafanya vyakula vya mifugo kuwa ghali sana na inalipiwa mara mbili, wafugaji inawabidi wakati wananunua chakula hicho wanalipa VAT wakati tayari watengezaji walikwishalipia wakati wananunua vichanganyio.

### a. Ukame na vifo vya mifugo

**Mheshimiwa Spika,** ukame uliopitiliza umeacha majanga makubwa kwa wafugaji katika maeneo mengi ya nchi hii, Kambi Rasmi ya Upinzani imepata baadhi ya taarifa

za wafugaji ambao wamepoteza mifugo yao na wengine kufikia hatua ya kujiua kutokana na hasara waliyoipata.

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni baadhi ya maeneo yaliyoathirika na ukame na kupoteza mifugo;

*Mkoani Morogoro, zaidi ya ng'ombe 15,000 wamekufa katika vijiji vitano wilayani Mvomero kutokana na ukame. Katika vijiji vya Dakawa, Sokoine, Kambala,Mera na Melela, baadhi ya wafugaji wakilalamikia mifugo yao kuanguka na kufa baada ya kukosa chakula na maji.*

*Katibu wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Morogoro, Kochocho Mgema, alivitaja vijiji vilivyoathirika zaidi na ukame na idadi ya ng'ombe waliokufa kwenye mabano ni Dakawa (2,723), Sokoine (4,246), Kambala (1,328), Mera (1,284) na Melela (1,057).*

*Kwa upande wa Wilaya ya Kilosa, zaidi ya ng'ombe 3,328 wamekufa.*

*Mfugaji katika Kitongoji cha Chaua, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Chalinze, Hamisi Meya, amepoteza ng'ombe zaidi ya 100, ndugu Karanga kutoka Mdaula, Bagamoyo, akipoteza ng'ombe 220.*

***Mkoa wa Manyara:*** *Simanjiro kata zilizoathirika na ukame kwa kiasi kikubwa ni Remiti, Losoboit, Kitwai na Leseinyai. Monduli ni Mswakini, Lokisale, makuyuni n.k. Kiteto ni Lengatei, Sunya, Laiseri, Lorela na Kijungu.*

**Mheshimiwa Spika,** kuna wafugaji wengi kutoka mkoa wa manyara, Dodoma na maeneo mengine ya wafugaji ng'ombe wao walikufa kutokana na ukame uliopitiliza. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako na wafugaji ni hatua gani za makusudi za kuhakikisha wafugaji waliopoteza mifugo yao wanafidiwa kwa kupatiwa mitamba bora ili waendelee na maisha yao ya kawaida?

**Mheshimiwa Spika,** mbali na ukame huo ulioathiri kwa kiasi kikubwa ufugaji wa kuhamahama, lakini kuna matatizo ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iyape kipaumbele kama kweli inathamini mchango wa sekta hii, nayo ni;

1. Kufanya ushawishi kwa jamii kuhusu maeneo yaliyobainishwa ambayo yanaweza kutengwa kwa ajili ya wafugaji ili kuondoa migogoro ya ardhi iliyopo sasa baina ya wakulima na wafugaji.

2. Suala la upigaji chapa mifugo bado elimu haijatolewa kwa wafugaji na kupelekea malalamiko mengi sana toka kwa wafugaji. Wizara ilisitisha kuanza zoezi hilo lakini baadhi ya mikoa kama Morogoro na Singida wilaya ya Manyoni zoezi linaendelea kwa nguvu.

3. Kamata kamata ya mifugo na unyanyasaji mkubwa wa wafugaji karibu nchi nzima usitishwe. Mfano huko Kagera mifugo inapigwa mnada kila siku na kuwaacha wafugaji wakiwa maskini kabisa. Pia kuwaondoa bila kuwaonyesha maeneo mbadala ya kupeleka mifugo yao inaongeza migogoro ya
ardhi na baina yao na watu wanaowakuta tayari kwenye maeneo wanapokwenda. Maeneo ya Pwani ambapo wafugaji wameuawa bila kuwa na kosa lolote- Mfano, Waziri wa mambo ya ndani alipowaomba wafugaji wa Kibarbaig wawazike wapendwa wao waliouwawa na Polisi.

## b. Mapitio ya Bajeti ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2015/16 Idara kuu za mifugo na uvuvi haikupokea fedha yoyote toka ndani bali ilipokea fedha za nje jumla ya shilingi

**547,375,920/-**. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Fungu 99 ilitengewa na bunge jumla ya shilingi **60,013,252,440.56/-** na kati ya fedha hizo shilingi **15,873,215,000/-** (fedha hizi zimejumuisha Mifugo & Uvuvi) zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2016/17, sekta hii ya mifugo imetengewa shilingi **4,000,000,000/-** tu (kwa ajili ya huduma ya mifugo, na uzalishaji wa mifugo), kati ya fedha hizi ni shilingi **130,000,000/-** tu ndizo zilizotelewa kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa kuna umuhimu wa sekta ya mifugo kuboreshwa na kupewa kipaumbele katika uzalishaji na soko; aina ya mifugo, aina ya ufugaji na masoko.

## V. SEKTA YA UVUVI: Fungu 64

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya uvuvi namba 22 ya 2003 ina kasoro na inatia mashaka kama wakati wa kutungwa kwake ulifanyika utafiti wa kina na kuhusisha wadau wote (hasa wavuvi).

- Sheria hiyo inataka nyavu zote za samaki aina ya dagaa ziwe na upana wa matundu wa 10 mm lakini ukweli ni kwamba dagaa wanaopatikana katika ziwa Tanganyika ni tofauti na Ziwa Nyasa na ni

tofauti na Ziwa Vitoria na hata wale wa bahari ya Hindi. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuifanyia rejea Sheria hiyo ili wavuvi wa Dagaa katika Ziwa Viktoria wasiendelee kuchomewa nyavu zao za kuvulia dagaa kwa kuwa haziko kwenye viwango vya kisheria.

- Sheria inataka nyavu za Sangara kuwa na "piece" moja badala ya kuunganishwa hadi "piece" tatu. Kwa kutumia "piece" moja kwa wavu kunawa lazimisha wavuvi kuvua kwenye kina kifupi na hivyo kuharibu mazalia ya samaki tofauti na kama nyavu hizi zingeunganishwa ambapo wavuvi wataweza kuvua katika maji ya kina kirefu na hivyo kutovuruga mazalia ya samaki.

**Mheshimiwa Spika,** badala ya kutumia nguvu kubwa kuchoma nyavu, Serikali itoe fursa za mikopo kwa wavuvi na kutoa elimu ya ufugaji wa samaki, pia kuweka mpango mzuri wa matumizi ya ziwa na Bahari. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa unapomchomea mvuvi nyavu na zana nyingine za uvuvi bila kuwapa wavuvi hawa njia mbadala wa kufanya shughuli zao ni kutoondoa tatizo na kusababisha shida kubwa ya maisha kwa watu hawa.

**Mheshimiwa Spika,** Wavuvi wanakabiliwa na tozo nyingi sana ambazo zinaathiri kipato chao. Wavuvi wana tozo zaidi ya (tisa) 9 kulingana na maeneo wanayofanyia shughuli zao. Tozo hizi ni kama vile: Ada ya SUMATRA,

leseni ya uvuvi, zimamoto, maegesho, leseni ya mtumbwi, kodi chini ya TRA, leseni ya usafirishaji n.k.

Pamoja na hapo, leseni ya mtumbwi;

a. Hutozwa kwa kiwango sawa bila kuangalia ukubwa wa mtumbwi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Mitumbwi itozwe kulingana na ukubwa.
b. Mitumbwi ukishalipiwa tozo ya leseni, basi itambuliwe mahala popote katika ziwa husika badala ya kila eneo kutoza tozo yake.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa usalama katika maziwa jambo linalopelekea wavuvi kuvamiwa mara kwa mara na kunyang'anywa zana zao za kazi, na wakati mwingine watu hawa hujeruhiwa na hata kuuwawa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kufuatilia suala hili na kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha ulinzi na usalama katika 'madago'

**Mheshimiwa Spika**, elimu ya ufugaji wa samaki (aquaculture) kama ingetolewa vyema lingekuwa ni jambo ambalo lingepunguza uvuvi haramu katika maziwa na bahari, na pia ni fursa nzuri ya kuongeza kipato kwa wafugaji samaki.

**Mheshimiwa Spika,** kuna umuhimu mkubwa sana katika kuboresha na kusimamia shughuli na miuondo mbinu za uvuvi na rasilimali zake. Katika mwaka 2016/17 ni shilingi **544,461,000/- tu** zilitengwa kwa ajili ya shughuli za doria.

Lakini hadi mwezi machi, 2017 zilitolewa shilingi **108,792,464.** sawa na shilingi 20.

### a. Mapitio ya Bajeti ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** fedha zilizotolewa wa mwaka 2016/17 kwa matumizi ya maendeleo ya uvuvi ni shilingi **5,369,160,000/-** tu (shilingi 4,369,160,000/- kati ya hizi ni fedha za nje kutoka mradi wa SWIOFish). Kiasi hiki cha fedha ni kidogo sana.

## VI. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya kilimo, kwa muktadha mzima wa sekta nzima ya mazao na visaidizi vyake, sekta ya mifugo pamoja na sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana na ndiyo sekta ambayo kwa upana wake inayotoa ajira nyingi kwa watanzania wa makundi yote, takwimu za mwaka 2014 sekta inatoa ajira kwa asilimia 66.9[6].

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wake katika suala zima la kiuchumi ili Tanzania iweze kutekeleza vyema mpango wake wa pili wa miaka mitano wa maendeleo, haina budi kujikita katika kuhakikisha inatoa fedha za maendeleo kwa sekta nzima kama ambavyo wataalam walivyopanga na baadae Bunge hili kupitisha. Kwa kuwa tayari Bunge lilikwisha toa Baraka za utekelezaji wa mpango huo na hivyo kuwa ndiyo dira

[6] National Five year Development plan 2016/17-2020/21, pg.55

kwa kila mpango wa maendeleo hadi pale miaka mitano itakapo malizika, hivyo basi, kitendo chochote cha Serikali kutoufuata mpango huo; Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo kuwa ni Serikali kulidharau Bunge au kulidanganya Bunge kwa kuleta taarifa ambazo hazina uhalisia na hivyo kushindwa/ kukataa kwa makusudi kufuata kile walichokipanga.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, kwa “trend”ya utoaji wa fedha kwa sekta hii ni dhahiri Tanzania kuwa nchi ya viwanda na hivyo kuwa na uchumi wa kati itakuwa ni njonzi za mchana.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

……………………………………………………

**Dr. Sware I. Semesi (Mb)**
**Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**
**Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**
**19.05.2015**